

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P. 20,
MISUNGWI

Simu: 255-732980745
Fax: 255 732980745



BaruaPepe: dedmisungwi@gmail.com

Unapojibu tafadhali taja

Kumb Na. MZA/MDC/S.10/35/35

26/03/2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri uya Wilaya ya Misungwi anawaangazia nafasi za kazi Wananchi wote wenye sifa baada ya kupokea Kibali cha ajira mpya kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora cha tarehe 22 Agosti 2017 chenye Kumb.Na.CFC 26/205/01.FF/91 ambacho kimeongezewa muda wa utekelezaji na Kibali cha tarehe 12 Machi 2018 chenye Kumb.Na.CFC.26/205/01.GG/95 kwa Watendaji wa Vijiji Daraja la III.

I. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 60)

A. SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na cheti cha kuhitimu na kufauru kidato cha nne(Frm IV) au Kidato cha sita (Frm VI).
- Awe amehitimu Mafunzo ya Cheti/Astahada kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali katika fani ya Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa.
- Awe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka arobaini na tano (45)

B. MAJUKUMU

- Atakuwa Mtendaji na Mshauri Mkuu wa Serikali ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya maendeleo na utekelezaji wa mipango ya maendeleo.
- Atasimamia masuala yote ya Ulinzi na Usalama katika ngazi ya Kijiji
- Atakuwa Afisa Mhasibu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Serikali ya Kijiji.
- Atakuwa Katibu wa Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- Atatafsiri Sera, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo ndogo za Halmashauri ya Kijiji.

- Ataratibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuziwasilisha kwenye Halmashauri ya Kijiji na baadaye kwenye Kata.
- Atasimamia matumizi bora ya nguvu kazi.
- Atasimamia ukusanyaji wa kumbu kumbu za Walipa kodi, Wataalam mbali mbali na NGOs waliopo katika ngazi ya Kijiji.
- Atasimamia matumizi bora ya nguvu kazi.
- Atakuwa Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji.
- Atatekeleza majukumu mengine atakayopangiwa na Mkurugenzi Mtendaji(W).

C. NGAZI YA MSHAHARA

- Mwajiriwa atalipwa Mshahara katika viwango vya Serikali yaani TGS B sawa na Tsh.390,000/= kwa Mwezi.

D. MASHARTI YA JUMLA

- Mwombaji awe hajawahi kupatikana na hatia ya kosa la jinai au kufungwa jela.
- Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya Taaluma na Mafunzo, Maelezo binafsi (CV), Cheti cha kuzaliwa, pamoja na picha mbili za rangi (Passport Size).
- Matokeo ya masomo (provisional results) havitakubaliwa.
- Taarifa zozote za kughushi ambazo zitawasilishwa na mhusika, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
- Watakaochaguliwa kuhudhuria Usaili watafahamishwa kwa njia ya simu na barua kupitia anuani zao walizotumia.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **09 April 2018** saa **9.30 alasiri**.
- Maombi yote yatumwe kupitia Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 20,
MISUNGWI.
MWANZA.

Imetolewa na,


Frederick Nyoka

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MISUNGWI

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA